# TUICO YATIMIZA MIAKA 30

## RISALA YA CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI (TUICO) KWA MGENI RASMI WAKATI WA UZINDUZI WA MIAKA 30 YA TUICO NA KITABU CHA MAFUNZO MUHIMU KWA WAFANYAKAZI TAREHE 02 JUNI, 2025 KATIKA UKUMBI WA MORENA HOTEL MJINI MOROGORO

Mheshimiwa Mgeni Rasmi Mh. Ridhiwani Kikwete (Mb.) Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu),
Mheshimiwa Kamishna wa Kazi
Mheshimiwa Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri,
Mheshimiwa Mkurugenzi Mkuu wa CMA
Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro
Mheshimiwa Mkurugenzi Mkuu wa NSSF
Ndugu Mwenyekiti wa TUICO Taifa
Ndugu Viongozi wote mliopo hapa itifaki imezingatiwa

Awali ya yote tunapenda kumshukuru Mungu mwingi wa Rehema kwa upendo wake mkuu uliotuwezesha uzima na Afya hatimaye tumeweza kukutana siku hii ya leo Mjini Morogoro.

Pili Chama kinapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukuamini na kukuteua wewe kuwa Waziri mwenye dhamana katika masuala ya Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu nasi tunakupongeza na tunaahidi kushikirikiana na wewe binafsi Pamoja na Wizara unayoiongoza.

Tatu, Chama kinapenda kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kwako kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii ya Uzinduzi wa miaka 30 ya TUICO sambamba na Kitabu cha Mafunzo Muhimu kwa Wafanyakazi. Tunatambua kuwa una majukumu makubwa ya ujenzi wa Taifa, hata hivyo ukaona ni vema ushiriki nasi. Chama kinakushukuru sana.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Chama cha Wafanyakazi TUICO kiliundwa rasmi mwaka 1995 kufuatia Mkutano Mkuu uliofanyika jijini Arusha. Mpaka kufikia mwaka 2025 Chama kimetimiza miaka 30 ya uhai wake.

Katika kipindi cha miaka 30 Chama kimepata mafanikio makubwa kwani kilipoanza kilikuwa na Wanachama 30,000 ambao kiliwarithi kutoka OTTU na kilikuwa na Sekta mbili tu yaani Sekta ya Viwanda na Biashara.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Katika miaka 30 Chama kimepata mafanikio makubwa ambayo kwa muda huu mfupi ni vigumu kuyaorodhesha yote. Hata hivyo kwa kifupi ni kama ifuatavyo:-

1. Uwepo wake mpaka sasa ni mafanikio makubwa

2. Chama kimehamasisha Wafanyakazi kujiunga na Chama na sasa kina wanachama 150,000

3. Chama sasa kinahudumia Wanachama katika Sekta nne ambazo ni:-

(a) Viwanda
(b) Biashara
(c) Taasisi za Fedha
(d) Huduma na Ushauri

4. Chama kina ofisi katika Mikoa mikubwa 22, Ofisi ndogo tano (5) na Ofisi ya Makao Makuu. Ofisi zote zina watumishi wa kutosha wenye weredi na vitendea kazi ikiwemo usafiri wa uhakika hivyo huduma kuwafikia wanachama katika ubora mkubwa na unaokubalika.

5. Chama cha Wafanyakazi TUICO kinaongoza kwa kufunga Mikataba ya Hali Bora za Kazi. Chama kimefikia uwezo wa kufung aMikataba kati ya 80 – 100 kwa mwaka. Mikataba hii huboresha maslali ya Wafanyakazi mahala pa kazi.

6. Ndugu Mgeni Rasmi, Chama cha Wafnyakazi TUICO kimekuwa mstari wa mbele kutatua migogoro ya Wafanyakazi mahali pa kazi katika ngazi mbalimbali za kutoa haki. Chama kimekuwa kikipokea migogoro takribani 320 kwa mwaka. Kupitia Chama Wafanyakazi wengi hupata haki na maslahi yao.

7. Chama kimekuwa kikitoa mafunzo kwa Wafanyakazi, Wanachama na Waajiri juu ya masuala ya Vyama vya Wafanyakazi. Kwa sasa Chama huendesha semina zaidi ya 10,000 kwa mwaka. Semina hizi huwajengea uwezo washiriki na kupunguza migogoro mahali pa kazi.

8. Chama kimeendelea kujenga uhusiano mwema na Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kama TUCTA, ATE, ILO, FES, IndustriAll, PSI, DTDA, FNV, BWI, IUF na Mashikikisho mengine Duniani. Chama kimepata uzoefu mkubwa katika uendeshaji wa shughuliu za Vyama vya Wafanyakazi.

9. Ndugu Mgeni Rasmi, Kupitia ushirikiano huo, Chama kimeendelea kunufaika na kupata matunda mazuri yatokanayo na Uongozi mzuri wa Mheshimiwa Dkt, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi cha awamu ya sita, tumeshuhudia Serikali ikiboresha kwa kiasi kikubwa maslahi ya Wafanyakazi kwa kuboresha mishahara, kupandisha madaraja, kuboresha Mafao ya Wastaafu, kuwajali na kuweka mazingira mazuri kwa wakina mama wanaojifungua Watoto Njiti na kuboresha sheria mbalimbali zinazowagusa wafanyakazi hapa Nchini.

10. **Ndugu Mgeni Rasmi**, Chama kinashiriki kikamilifu tangu kuanzishwa kwake katika taasisi za utatu kama vile Tume ya usuluhishi na Uamuzi (CMA) Bodi za Kima cha Chini cha Mshahara (Wage Boards) Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii (LESCO), Kamati ya Huduma Muhimu (Essential Services Committee) na Bodi Mbalimbali katika Taasisi za Umma, hivyo kuimarisha utatu wetu.

11. **Ndugu Mgeni Rasmi,** Chama kinatambua umuhimu wa mafunzo kwa Wafanyakazi na Wanachama wake, kwa kutambua umuhimu huo Chama kimeandaa **KITABU CHA MAFUNZO MUHIMU KWA WAFANYAKAZI.** Kitabu hiki

kitatumika kama mwongozo wa kupata maarifa juu ya Vyama vya Wafanyakazi Nchini. Aidha Wafanyakazi, Wanachama, Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi katika ngazi mbalimbali Waajiri, Wanazuoni na Wadau mbalimbali watanufaika na elimu iliyotolewa katika kitabu hiki.

**Ndugu Mgeni Rasmi**, pamoja na mafanikio haya Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) katika uhai wake wa miaka 30 kilikabiliana na changamoto mbalimbali katika utoaji wa huduma kwa wanachama. Hivyo tunafurahi kwamba katika kukabiliana na changamoto tuliweza kuimarisha Umoja na Mshikamano na kulinda haya mafanikio yaliyopo sasa.

Hata hivyo, katika kuendelea kutatua changamoto tulizonazo, tunaiomba Serikali;-

1. Kuwaelekeza baadhi ya Waajiri wasiopenda uwepo wa Vyama vya Wafanyakazi mahala pa kazi kuviruhusu Vyama hivyo kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria sambamba na kuwaruhusu Wafanyakazi Nchini kutumia uhuru na zao kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi.

2. Kutoa nafasi za uwakilishi wa Wafanyakazi katika Bodi za Taasisi na mashirika mbalimbali ya Umma.

3. Kuwahamasisha waajiri kutoa wigo wa majadiliano ya Pamoja, kufunga na kutekeleza Mikataba ya Hali ya Bora za Kazi.

4. Kuhakikisha wanatengeneza mazingira rafiki ya kazi ikiwemo suala la Afya na Usalama mahala pa kazi.

Mwisho Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) kitaendelea kushirikiana na Serikali na wadau mbalimbali kuhakikisha kuwa Haki, Maslahi na Heshima ya Wafanyakazi inalindwa.

Mshikamano Daima!